Students Name: ..................................................................................

School Name................................................... Index Number ..............

**P320/1**
**FASIHI YA KISWAHILI**
Paper 1
Saa Tatu.
JULAI./AGOSTI

# HES MOCK EXAMINATIONS 2025

## UGANDA ADVANCED CERTIFICATE OF EDUCATION

## FASIHI YA KISWAHILI

**(NATHARI NA USHAIRI)**

**KARATASI YA KWANZA**

**SAA TATU**

**MAAGIZO**

- Karatasi hii Ina sehemu tatu, **A**, **B** Na **CH**. Mtahiniwa anapaswa kujibu sehemu zote. Katika sehemu **CH**, mtahiniwa achague Diwani moja Tu.
- Maswali ya ziada yatakayojibiwa hayatasahihishwa

## SEHEMU A

1. Soma kifungo kifuatacho kasha ujibu maswali yanayofuata.

Mateso ya wanawake ni suala la kijamii linatofaa kutazamwa kwa darubini kali.

Hata hivyo wanawathirika zaidi ni watoto ambao bado wako katika umvi unaohitaji kuelewa na kupewa mahitaji ya msingi kama mavazi, malazi, elimu na mengine anuai.

Hali ya kuachwa na wazazi imekuwa ikizikimba jamii tangu enzi za mababu na kila itokeapo. Wanajamii huipokea kwa mitazamo, hivyo kuwafanya wanawakiwa kuathirika sana.

Baadhi ya jami zina imani za kijadi pamwe na mila zilizochkaa zinazozifanya kuamini kuwa baadhi ya vifo hutokana na laana.

Wengine huchukulia kuwa mwendazake ameondolewa na ulozi.

Imani kama hizi huifanya jamii kuwatia watoto walioachwa katika mkumbo uleule, hivyo kuwangalia kwa macho ya kawaida.

Hili husababisha dhana gande. Hali huasababisha kuwachukulia watoto kama wanao toka katika kizazi kilicholaaniwa. Jami basi hukosa kuwapa watoto hawa stahiki yao. Hata wanapohitaji kujitahidi kuwania nafasi yao, waliowowazunguka huwavunja mioyo. Jitihada zao huishia kuwa si chocolate kwa kuwa jami inawatazama kama waliolaaniwa.

Punde baada ya mzazi mmoja au wote wawili waendapo wasikovudi, inatarajiwa kwamba aliyeachiwa mtoto awe mzazi wake, mwanafamilia au jirani awajibike na kumtunza mwanamkiwa. Kunao kadha wa kadha wanaowajibika – ninawavulia kofia. Hata hivyo wengi hutekeleza jukumu hili walilipewa na muumba.

Si ajabu basi kuona kuwa idadi ya watoto wanaozuvura mitaani inazidi kuongezeka kila uchao. Ukichunguza utakuta kuwa wengi wa watoto wanaozuvuva mitaani ni waliopotelewa na wazaza wao.

Inakeva zaidi kugundua kuwa baadhi ya watoto hawa wana mzazi mmoja. Kwamna mke au mume wa mtu ameaga, au iwe kwamba mzazi mmoja alimzaa mtoto na kumwachia mwenzake mzigo wa ulezi.

Aliyeachiwa ana jukumu la kumpa mwanawe mahitaji yoyote muhimu/msingi. Machoni pa Jalali, kila anayepuuza wajibu huu anahukumu yake siku ya kiama! Ni haki ya kila mtoto kupata elimu. Katika katiba yetu mathalan, elimu ya msingi, yaani kuanzi shule ya chekechea hadi kidato cha nne ni ya lazima.

Tangu hap hata hivyo, jamii zimekuwa zikiwanyima wanawakiwa wengi elimu. Kwamba kunao wachache wanaowaelimisha baadhi ya wanawakiwa ni kweli.

Hata hivyo, wengi hukosa hata wa kuwapeleka katik shule ya chekechea, hivyo kuishia kutojua hata kutojua hata kuandika majina yao.

Mfikivie mtu katika kerne ya 21, asiyejua kusoma wala kuandika! Nani ajuaye huenda huyo mwanamakiwa siyepelekwa shuleni ndiye angalikuwa profesa, daktari, mwalimu, rubani, anu msomi mtajika na mtaalamu wa uwanja muhimu katika jami!

Kila mtoto ana haki ya kuelewa hadi kufikia utu uzima kabla ya kupewa majukumu mazito. Katika katiba yetu, utu uzima, ulio umvi wa kuanza kufanya kazi huanzia miaka 18.

Wanaohakikisha watoto hawa wametimiza utu uzima kabla ya kufanyishwa kazi ngu… wamafaa pongezi. Hata hivyo wana wakiwa wamekuwa wakituniwa na wengi kama punda wa huduna.

Wanaaila wengine huwachukuwa wanawakiwa kwa machozi mengi. Wazazi wao waagapo na kuapa kuwahitadhi na kuwatunza wana wale wa ndugu zao, kumbe ni machozi ya samba kumlilia swara! Hata kabla ya mwili wa mzazi mhusika kuliwa na viwari, mateso kwa mtoto Yule huanza, akawa ndiye afanyaye kazi zote ngumu.

Utakuta watoto wao wamekaa kama Sultan bin Jerere huku mwanamkiwa Yule akiwapikia, kuwafulia nguo, kudeki, karibu hata kuwaosha miili! Kazi kama zile za shokoa huwa za suhubu na angalabu husindikizwa kwa matusi yasiyoandikuka.

Baadhi ya waja walionyimwa huruma huwahadaa wanawakiwa na kuwapeleka ngambo wakitumia vyambo, kuwa wakifika kule watapata kazi za kifahari.

Maskini wale husihia kushikwa shokoa, wakawa watumwa katika nyumba za waajiri wao, bila namna ya kujinasua. Wengine huishia kutumiwa kama watumwa wa kimapenzi katika madanguro, miili yao ikawa ya kuuziwa makahaba waroho wasigali utu.

Kujinasua kule huwa sawa na kujitahidi kuokoa ukuni uliokwishageuka jivu, maadamu wanawakiwa adhalabu hukosa watu wenye mioyo ya huruma ya kuwashughulikia.

Wengi hutumiwa methali mwana wa ndugu kirugu mjukuu mwanangwa. Kuwa puuzilia mbali wanawakiwa ambao hukimbiliwa tu wabinafsi hawa wanapofandika wenyewe.

**MASWALI:**

(a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka (Alama 04)
(b) Eleza dhana ya mwanamkiwa kwa mujibu wa kifungu hitu. (Alama 04)
(c) Eleza imani za kijadi kuhusiana na wanwakiwa. (Alama 06)
(d) Jadili masaibu yanayowakumba wanawakiwa (Alama 10)
(e) Eleza haki za kikatiba zilizokiukwa kuhusiana na wanawakiwa (Alama 04)

(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na kifungu

(a) Inakera

(b) Majukumu

(c) Mwana wa ndugu kirugu mjukuu mwanangwa

(d) Kuokoa ukuni uliokwishageuka jivu

*(e)* Kushikwa shokoa. (Alama 05)

**SEHEMU B.**

2. Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali.

Siku ilikuchaa vibaya kwamvua, ngurumo na makeke ya umeme. Kwa hali hii, kila mahluki alilazimika kwenda kulala mbele ya saa ya kawaida.
Mmuliko mmoja ulipenya nyumbani mwangu, mkawa mweupe kama mlikuwa na taa ya umeme. Dakika ileile nilisikia mnazi ulioko uwani ukianguka, na mbele barazani nilisikia kitu kikichugachuga, ambacho nilituhumu kwamba kitu hicho kilikuwa kinabari mvua. Dhaana zangu zaliniambia kuwa ni nyamaume mawindoni. Basi nikaupinda mgoroli wangu toka unyayoni hadi utosini, na mara tu nikalala.

Asubuhi yake kulikuwa shwari, na jua lilionekana kuwa kali ingawa ilikuwa saa kumi na mbili na nusu tu nilipoamka. Basi nilikwenda kufungua mlango huku moyo ukinisisimka.Kule kufungua tu, nikaona nyama kubwa limekingama mlangoni. Dakika ileile, nilifunga mlango kwa hofu na kuduwaa, nikisikiliza moyo ukinidunda. Nilidhani ni simba kama nilivyokisia jana usiku. Halafu nikafafanua jinsi nilivyomwona tena, nikakumbuka kuwa nilimwona na hatamu na saruji, naling'amua kwamba hakuwa simba.

Basi, nikafungua mlango tena, nayule mnyama akanilaki, kwa huzuni, huzuni, huku akikaza machoyake katika maiti iliyokasimiwa na kitu Fulani, na iliyolala pale uwani pangu. Kwamba nyumba yangu ilikuwa karibu na barabara, nilifahamu kwamba msafiri Yule alikuwa akija kwangu kubari mvua na kuepa dhoruba ile ya jana usiku, alipopatikana na mkasa ule. Ama kweli yake ilikuwa bahati mbaya, kwani mbwa hafi maji aonapo ufuko. Maskini Kisigino sikuwa na la kufanya kwa muda wa nusu saa nzima kwa butwaa lililonipiga.

**MASWALI**

i) Kwa kutoa mifano kutoka hadithi, taja fani mbili za lugha mwandishi alizotumia. (Alama 06)

ii) Eleza toni ya mwandishi kutokana na maelezo katika hadithi. (Alama 05)

iii) Ni sifa zipi msimulizi anazopewa kutokana na kisa anachosimulia? (Alama 06)

iv) Msomaji wa hadithi hii anapata hisia zipi? (Alama 04)

v) Fafanua muktadha wa hadithi. (Alama 04)

vi) Ni dhamira gani inayojitokeza katika hadithi? (Alama 08)

**SEHEMU CH; USHAIRI;**

**WALLAH BIN WALLAH: MALENGA WA ZIWA KUU**

3. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yatakayofuata hapo chini;

**UNAFIKI**

Tafutani usalama:
Kunyamanza sitoweza, naona bora kusema
Niketile nikiwaza, fitina si mtu mwema
Wengi wamejipoteza, husalia kulalama
Hakuna haja kuzoza.

Tafutani usalama:
Leo nitawadokeza, nanywi mpate yapima
Fatani ahilikiza, na mbaya hana mema
Kama wapinga uliza, masheha waliosoma
Hakuna haja kuzoza

Tafutani usalama:
Uache kumpongeza, hasidi hana heshima
Wengi wameteketeza, kwa maneno nyuma nyuma
Ni bora kumfukuza,aondoke hima hima
Hakuna haja kuzoza.

Tafutani usalama:
Basi fitina punguza, uwaze mbele na nyuma
Dunia ni mageuza, tego hili utakwama
Kwa janga ulilovyanza, ukidhani unachuma
Hakuna haja kuzoza.

Tafutani usalama;
Nia yangu si kuzoza, wala sitaki lawama
Tangazo ninatangaza, tuishi pasi hasama
Fitina haina jaza, ni ujinga si ulama
Hakuna haja kuzoza.

Tafutani usalama:
Tama hapa nanyamanza, kwenda mbele kwanilema
Fatani hela sikiza, kuna siku utahema
Mno unajiumiza, upoteze na uzima
Hakuna haja kuzoza.

**MASWALI**

(a) Shairi hili lina urari upi?. (Alama 06)

(b) Kulingana na shairi hili, wewe kama mtahiniwa unapata ujumbe gani? (Alama 04*)*

(c) Ni nini hasa lengo kuu la mshairi katika shairi hili? (Alama 02)

(d) Chambua muundo wa shairi hili. (Alama 08)

(e) Ukirejelea mifano kutoka shairi hilo, eleza jinsi malenga anavyotumia mbinu zifuatazo; (Alama 06)

i) Inkisari.
ii) Mazida.
iii) Kuboronga sarufi.

f) Tambua bahari angalau nne zilizomo katika shairi hili. (Alama 08)

4. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali yatakayofuata.

Leo nawambia "hembu" nipatieni kalio.
Ninene naye mbumbumbu, wa kutojua upeo.
Eti azuia mumbu, yaoleni makulio.
Yaoleni makulio, eti azuia mumbu.

Yundani ya kiminyano, mikono ni yake ngao.
Kasiga hana usono, kwa majasho na kupuo.
Haetuki kwa hilino, yu katika angamio.
Yaoleni makulio, eti azuia mumbu

Mumbu hasinua miti, yenye vimo na matao.
Si mno kupitwa kati, madharae ni kilio,
Uwe maji ya magoti, sisi hatunyeti nao.
Yaoleni makulio, eti azuia mumbu

Huko juu ushukapo, ni yowe na makamio,
Pili kila kilichopo, si masiki si mabao.

Hakiachwi ila hapo, hufanya maandamio.
Yaoleni makulio, eti azuia mumbu

Ni vipi huyu mwenzetu, akatekwa na kileo.
Ajivika hana matu,kwa wingi wa bambalio,
Atakula mtukutu, asambe ni mwendeleo,
Yaoleni makulio, eti azuia mumbu

Jinsi alivyotuna, katika hili tukio,
Lau kwamba twamnena, jawabule ni mkao,
Heri njia kugawana, kila mtu ende kwao,
Yaoleni makulio, eti azuia mumbu

**MASWALI**

a) Kwa kutoa mifano kutoka shairi 'MZUIA MUMBU', eleza maana ya kila isitilahi uliyopewa chini.

(i) Inksari (Alama 03)
(ii) Tabdila (Alama 03)
(iii) Mazida (Alama 03)
(iv) Kibwagizo (Alama 03)
(v) Vina (Alama 03)

b) Eleza mafunzo msomaji wa shairi la 'MZUIA MUMBU' anayopata. (Alama 08)

## SHIHABDIN CHIRAGHDIN: MALENGA WA KARME MOJA

5. Soma shairi hili na kisha ujibu maswali yanayofuata.

**Tozi lanilengalenga**

Tozi hunilengalenga, katika ndani
Kiwakumbuka malenga,wale wendani
Wasufiwe na matanga, ni maskini
Ziba panapo utoto, wale pasiwe penyepenye

Upazoibe kwa mpato, upazibe pazibane
Kifunuwa langu ito, nipaone palingane
Akiya mtu asipaye, na apenyapo ni wazi

Ziwzni penye utoto, penye wazi, mpangaye

Mpapate kwa mpato, pasisalie penyepenye
Pitapo kivua mato, nipaone paligenye
Kiya mtu asipenye, na apenyapo ni waz

**MASWALI**

(a) Mtunzi anaongozwa na dhamira gani kulitunga shairi hili? (Alama 02)

(b) Kichwa cha shairi hili *Tozi linalengalenga* kinamaanisha nini? Fafanua ukilejelea shairi lenyewe (Alama 02)

(c) Kwa kutumia mifano, eleza aina ya muundo wa shairi hili. (Alama 06)

(d) Msiba uliowaangukia malenga unamwathiri vipi mshairi? (Alama 08)

(e) Changanua toni ya mshairi kulingana na shairi hili. (Alama 04)

(f) Uhuru wa mshairi umejitikezaje katika shari hili?fafanua huku ukirejelea mifano (Alama 06)

(g) Shairi hili linadhihirisha ujumbe gani kwa msomaji? (Alama 06)

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Kila msonga ugali, ndiye alaye makoko.
Name sioni muhali, chusa wala unguliko,
Hapa nilipo ni tuli, siingii papatiko,
Hayanidhuru makoko, ndimi msonga ugali.

Nayakwangua vizuri, kwa mabanzi na vijiko,
Haketi nje dhuhiri, walimwengu wangawako,
Hayala wamba futari, sharuba au bambiko,
Hayanidhuru makoko, ndimi msonga ugali.

Nala hayakomberesha, kisha hauramba mwiko,

Na nyungu nikaikosha, na jamii vilivyoko,
Sikimwi nikababakisha, hampa mwivu kicheko,
Hayanidhuru makoko, ndimi msonga ugali.

Wa kando hana lazima, kaletwa na mualiko,
Kuiza hanalo dhima, siteti simpi mwako,
Kwani dunia daima, I katika mizunguko,
Hayanidhuru makoko, ndimi msonga ugali.

Mgeni mkaribishwa, hangii ndani ya meko,
Majamvini hukalishwa, akakaachi kitako,
Eshapo akanawishwa, kwa maji mtiririko,
Hayanidhuru makoko, ndimi msonga ugali.

**MASWALI**

a) Chambua Maudhui yanayojitokeza katika shairi la 'MSONGA UGALI' (Alama 10)

b) Chambua umbo la shairi la 'MSONGA UGALI' (Alama 12)

ch) changanua toni la mshairi kulingana na shairi hili. (Alama 04)

d) Baada ya kusoma shairi hili, unapata hisia zipi? (Alama 08)

**MWISHO**